# Haki na Ulinzi Wako Dhidi ya Bili za Matibabu za Ghafla

Unapopokea huduma za dharura au unapotibiwa na mtoa huduma wa nje ya mtandao katika hospitali au Kituo cha Huduma za Upasuaji Usiohitaji Kulazwa Hospitalini kilicho ndani ya mtandao, umelindwa dhidi ya malipo ya salio. Katika hali hizi, hupaswi kutozwa zaidi ya gharama za mpango wako za malipo unayostahili kulipa mwenyewe, sehemu ya malipo ya bima unayopaswa kulipa na/au kiasi unachopaswa kukatwa.

## Je, "malipo ya salio" (ambayo wakati mwingine huitwa "malipo ya ghafla") ni nini?

Unapomwona daktari au mtoa huduma mwingine wa afya, huenda ukadaiwa gharama fulani za moja kwa moja, kama vile kiasi unachopaswa kulipa mwenyewe, sehemu ya malipo ya bima unayopaswa kulipa na/au kiasi unachopaswa kukatwa. Huenda ukawa na gharama za ziada au ukalazimika kulipa bili yote ukimwona mtoa huduma au ukitembelea kituo cha afya ambacho hakipo kwenye mtandao wa mpango wako wa afya.

Neno "Nje ya mtandao" linamaanisha watoa huduma na vituo ambavyo havijaweka saini ya mkataba na mpango wako wa afya kwa ajili ya kutoa huduma. Watoa huduma wa nje ya mtandao wanaweza kuruhusiwa kukutoza salio kati ya kiasi kinacholipwa na mpango wako na kiasi kamili kinachotozwa kwa ajili ya huduma fulani. Kiasi hicho kinaitwa "**malipo ya salio**." Kuna uwezekano kuwa kiasi hiki kinazidi gharama za ndani ya mtandao kwa ajili ya huduma ile ile na huenda kisihesabiwe kwenye gharama ya mpango wako ya kiasi unachokatwa au kiwango cha kila mwaka cha pesa unazolipa moja kwa moja.

"Malipo ya ghafla" ni malipo ya salio ambayo hukuyatarajia. Hali hii inaweza kutokea wakati huna uwezo wa kudhibiti wahusika wanaokupa huduma—kwa mfano wakati wa dharura au unaporatibu kutembelea kituo cha ndani ya mtandao lakini utibiwe na mtoa huduma wa nje ya mtandao bila kutarajia. Bili za matibabu za ghafla zinaweza kugharimu maelfu ya dola kulingana na utaratibu au huduma iliyotolewa.

## Umelindwa dhidi ya malipo ya salio kwa ajili ya:

### Huduma za dharura

Endapo utapatwa na tatizo la dharura la matibabu na upokee huduma za dharura kutoka kwa mtoa huduma au kituo cha nje ya mtandao, kiwango wanachoweza kukutoza ni kiasi cha malipo unachopaswa kulipa mwenyewe cha mpango wako cha za ndani ya mtandao pekee (kama vile kiasi cha malipo unachopaswa kulipa mwenyewe, sehemu ya malipo ya bima unayopaswa kulipa na kiasi unachopaswa kukatwa). **Huwezi** kutozwa malipo ya salio kwa ajili ya huduma hizi za dharura. Hii inajumuisha huduma ambazo huenda ukapokea baada ya kupata nafuu kidogo, isipokuwa ukitoa idhini iliyoandikwa ya kuondoa ulinzi dhidi ya kutozwa malipo ya salio kwa ajili ya huduma hizi za baada ya kupata nafuu.

Katika mwaka wa 2015, Connecticut ilipitisha sheria yao wenyewe kuhusu malipo ya salio. Sheria hiyo inatumika kwenye mipango ya afya inayodhibitiwa na Idara ya Bima ya Connecticut na ina ulinzi sawa na ule unaotolewa na Sheria ya nchi kuhusu 'Kuzuia Gharama za Ghafla'. Kwa maelezo zaidi, angalia Conn. Gen. Stat. §§ **38a-477aa** na **20-7f** au tovuti ya Idara ya Bima ya Connecticut katika **https://portal.ct.gov/CID/General-Consumer-Information/No-Surprises-Act.**

**Huduma fulani katika hospitali au kituo cha upasuaji cha ndani ya mtandao**
Unapopokea huduma kutoka hospitali au Kituo cha Huduma za Upasuaji Usiohitaji Kulazwa Hospitalini cha ndani ya mtandao, huenda baadhi ya watoa huduma pale wakawa wa nje ya mtandao. Katika hali hizi, watoa huduma hao wanaweza tu kukutoza kiasi cha malipo unachopaswa kulipa mwenyewe cha mpango wako cha ndani ya mtandao. Hii inatumika kwa dawa za dharura, nusukaputi, patholojia, rediolojia, maabara, neonatolojia, daktari msaidizi wa upasuaji, daktari wa huduma za hospitalini au huduma za wagonjwa walio katika hali mahututi. Watoa huduma hawa **hawawezi** kukutoza malipo ya salio na **hawawezi** kukuomba uondoe idhini yako ya kupata ulinzi dhidi ya kutozwa malipo ya salio.
Ukipokea aina zingine za huduma katika vituo hivi vya ndani ya mtandao, watoa huduma wa nje ya mtandao **hawawezi** kukutoza malipo ya salio isipokuwa ukitoa idhini ya kuondoa ulinzi wako kwa njia ya maandishi.

## Hutahitajika <u>kamwe</u> kuondoa idhini ya kupata ulinzi dhidi ya malipo ya salio. Aidha, huhitajiki kupata huduma kutoka nje ya mtandao. Unaweza kuchagua mtoa huduma au kituo katika mtandao wa mpango wako.

**<u>Pamoja na malipo ya salio kutoruhusiwa, pia unalindwa kwa njia zifuatazo:</u>**

- Unawajibika tu kulipa kiwango chako cha gharama (kama vile gharama za kiasi cha malipo unachopaswa kulipa mwenyewe, sehemu ya malipo ya bima unayopaswa kulipa na kiasi unachopaswa kukatwa, ambazo ungelipa iwapo mtoa huduma au kituo ni cha ndani ya mtandao). Mpango wako wa afya utalipa gharama zozote za ziada kwa watoa huduma na vituo vya nje ya mtandao moja kwa moja.

- Kwa jumla, ni lazima mpango wako wa afya:
    - Usimamie huduma za dharura bila kukuhitaji uidhinishiwe huduma mapema (hali inayojulikana pia kama "uidhinishaji wa awali").
    - Usimamie huduma za dharura kutoka kwa watoa huduma wa nje ya mtandao.
    - Ubainishe kiasi unachodaiwa na mtoa huduma au kituo (kugawana gharama) kulingana na malipo ambayo mpango wako ungetoa kwa mtoa huduma au kituo cha ndani ya mtandao na uonyeshe kiasi hicho katika ufafanuzi wa manufaa yako.
    - Uhesabu kiasi chochote unacholipa kwa ajili ya huduma za dharura au huduma za nje ya mtandao kwenye kiasi unachokatwa kwa huduma na kiwango chako cha malipo ya moja kwa moja cha ndani ya mtandao.

**Ikiwa unafikiri kwamba umetozwa malipo yasiyofaa,** wasiliana na Idara ya Bima ya Connecticut: **https://portal.ct.gov/CID/Consumer-Affairs/File-a-Complaint-or-Ask-a-Question** au Nambari ya Simu ya Usaidizi kwa Wateja: (800) 203-3447 au (860) 297-3900 au uwasiliane na Ofisi ya Mtetezi wa Huduma za Afya wa Jimbo la Connecticut kupitia 866-466-4446 au **Healthcare.advocate@ct.gov**.

Tembelea **www.cms.gov/nosurprises/consumers** ili upate maelezo zaidi kuhusu haki zako kwa mujibu wa sheria ya nchi.